
## MWELEKEO WA MSIMU WA MVUA ZA VULI (OKTOBA – DESEMBA), 2025 KWA MKOA WA KUSINI, PEMBA
**Umetolewa: 11/09/2025**

Taarifa hii inatoa mwelekeo wa msimu wa mvua za Vuli katika kipindi cha Oktoba - Desemba, 2025; athari na ushauri kwa sekta mbalimbali katika mkoa wa Kusini Pemba na wilaya zake:

### (I) Ngazi ya Mkoa




**Kielelezo 1: (a)** Mwelekeo wa msimu wa Vuli, 2025 kwa kisiwa cha Pemba. (b) Ramani inayoonesha wastani wa muda mrefu wa mvua za msimu wa Vuli katika sehemu mbalimbali za kisiwa cha Pemba. **Angalizo**: Wastani wa muda mrefu (miaka 30) wa mvua za mwezi Oktoba hadi Desemba, mabadiliko ya mvua kati ya mwaka mmoja na mwingine yamezingatiwa.

### Dondoo

*(i).* *Kwa ujumla mvua za Wastani hadi Chini ya Wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya mkoa wa Kusini Pemba.*
*(ii).* *Mvua zinatarajiwa kuanza wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Novemba, 2025.*
*(iii).* *Mvua zinatarajiwa kuisha mwezi Januari, 2026.*
*(iv).* *Vipindi vya ukavu vya siku kumi (10) au zaidi vinatarajiwa katika msimu huu wa Vuli.*

#### Mvua za msimu wa Vuli, 2025

Kwa ujumla mvua zinatarajiwa kuwa za Wastani hadi Chini ya Wastani katika maeneo mengi ya mkoa wa Kusini Pemba. Msimu unatarajiwa kutawaliwa na vipindi virefu vya ukavu na mtawanyiko usioridhisha.

***Angalizo:***
*Izingatiwe kuwa matukio ya hali mbaya ya hewa ikiwemo vipindi vya mvua kubwa yanaweza kujitokeza hata katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za Wastani hadi Chini ya Wastani.*


*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

(II) Ngazi ya Wilaya

## MWELEKEO WA MVUA ZA VULI (OKTOBA – DESEMBA), 2025 KWA WILAYA YA CHAKE CHAKE

**Umetolewa: 11/09/2025**

Taarifa hii inatoa mwelekeo wa mvua za Vuli katika kipindi cha Oktoba - Desemba, 2025 athari na ushauri kwa sekta za kilimo, mifugo na uvuvi katika wilaya ya Chake Chake.




Mwelekeo wa mvua za Vuli Oktoba-Desemba, 2025 kwa Wilaya ya Chake Chake, Kusini Pemba.

### Dondoo muhimu

*(i). Mvua za Wastani hadi Chini ya Wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya wilaya ya Chake Chake.*

*(ii). Mvua zinatarajiwa kuanza wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Novemba, 2025 na kutawaliwa na vipindi virefu vya ukavu na mtawanyiko wa mvua usioridhisha.*

*(iii). Mvua zinatarajiwa kuisha mwezi Januari, 2026.*

*(iv). Wakulima na wafugaji wanashauriwa kutumia mbinu bora za ufugaji na uzalishaji wa mazao ili kukabiliana na upungufu wa mvua.*

### Mvua za msimu wa Vuli, 2025 kwa wilaya ya Chake Chake

**Zitaanza:** Wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Novemba, 2025.

**Zitaisha:** Mwezi Januari, 2026.

**Kiasi cha mvua zinazotarajiwa:** Mvua zinatarajiwa kuwa za Wastani hadi Chini ya Wastani. Kwa kawaida wastani wa mvua katika miezi ya Oktoba - Desemba kwa wilaya ya Chake Chake ni kati ya milimita 320 hadi 380.

**Kiwango cha juu cha mvua:** Kinatarajiwa katika mwezi Desemba, 2025.

**Vipindi vya ukavu:** Upo uwezekano wa kutokea kwa vipindi virefu vya ukavu katika msimu huu wa Vuli, 2025.

**Ulinganifu:** Mvua zinatarajiwa kuwa chache na zenye mtawanyiko usioridhisha katika maeneo mengi ukilinganisha na Vuli iliyopita.

### Angalizo:

- **Wakulima, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kupata ushauri zaidi kutoka kwa maafisa ugani kwa matumizi sahihi ya taarifa za utabiri wa hali ya hewa.**

- **Watumiaji wa taarifa hii wanashauriwa kufuatilia utabiri wa saa 24, siku 10, mwezi pamoja na tahadhari kila zinapotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.**

### Matokeo na ushauri kwa kilimo, mifugo na uvuvi

#### Matokeo

(i). Upungufu wa unyevunyevu kwenye udongo katika maeneo mengi unaweza kuathiri uzalishaji wa mazao.

(ii). Vipindi vya ukavu vinaweza kupelekea kupungua kwa maji na hata kukauka kwa visima, hususan visima vifupi.

(iii). Upungufu wa mvua unaweza kuathiri upatikanaji wa malisho na maji kwa ajili ya mifugo

#### Ushauri

(i). Wakulima wanashauriwa kuandaa mashamba, kupanda, kupalilia na kutumia pembejeo husika kwa wakati na kuchagua mbegu na mazao sahihi.

(ii). Wakulima wanashauriwa kutumia mbinu bora za kilimo zinazohifadhi unyevunyevu katika udongo.

(iii). Wafugaji wanashauriwa kutumia mbinu bora za ufugaji ili kutunza malisho na kuvuna maji ya mvua kwa matumizi ya baadae.

(iv). Wafugaji wa samaki wanashauriwa kuimarisha miundombinu ya ufugaji.

Utabiri wa hali ya hewa nchini na tahadhari zinapatikana katika tovuti ya Mamlaka: **www.meteo.go.tz**


*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

(II) Ngazi ya Wilaya

## MWELEKEO WA MVUA ZA VULI (OKTOBA – DESEMBA), 2025 KWA WILAYA YA MKOANI

**Umetolewa: 11/09/2025**

Taarifa hii inatoa mwelekeo wa mvua za Vuli katika kipindi cha Oktoba - Desemba, 2025 athari na ushauri kwa sekta za kilimo, mifugo na uvuvi katika wilaya ya Mkoani.




Mwelekeo wa mvua za Vuli Oktoba-Desemba, 2025 kwa Wilaya ya Mkoani, Kusini Pemba.

### Dondoo muhimu

*(v). Mvua za Wastani hadi Chini ya Wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya wilaya ya Mkoani.*

*(vi). Mvua zinatarajiwa kuanza wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Novemba, 2025 na kutawaliwa na vipindi virefu vya ukavu na mtawanyiko wa mvua usioridhisha.*

*(vii). Mvua zinatarajiwa kuisha mwezi Januari, 2026.*

*(viii). Wakulima na wafugaji wanashauriwa kutumia mbinu bora za ufugaji na uzalishaji wa mazao ili kukabiliana na upungufu wa mvua.*

### Mvua za msimu wa Vuli, 2025 kwa wilaya ya Mkoani

**Zitaanza:** Wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Novemba, 2025.

**Zitaisha:** Mwezi Januari, 2026.

**Kiasi cha mvua zinazotarajiwa:** Mvua zinatarajiwa kuwa za Wastani hadi Chini ya Wastani. Kwa kawaida wastani wa mvua katika miezi ya Oktoba - Desemba kwa wilaya ya Mkoani ni kati ya milimita 320 hadi 380.

**Kiwango cha juu cha mvua:** Kinatarajiwa katika mwezi Desemba, 2025.

**Vipindi vya ukavu:** Upo uwezekano wa kutokea kwa vipindi virefu vya ukavu katika msimu huu wa Vuli, 2025.

**Ulinganifu:** Mvua zinatarajiwa kuwa chache na zenye mtawanyiko usioridhisha katika maeneo mengi ukilinganisha na Vuli iliyopita.

### Angalizo:

- **Wakulima, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kupata ushauri zaidi kutoka kwa maafisa ugani kwa matumizi sahihi ya taarifa za utabiri wa hali ya hewa.**

- **Watumiaji wa taarifa hii wanashauriwa kufuatilia utabiri wa saa 24, siku 10, mwezi pamoja na tahadhari kila zinapotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.**

### Matokeo na ushauri kwa kilimo, mifugo na uvuvi

#### Matokeo

(i). Upungufu wa unyevunyevu kwenye udongo katika maeneo mengi unaweza kuathiri uzalishaji wa mazao.

(ii). Vipindi vya ukavu vinaweza kupelekea kupungua kwa maji na hata kukauka kwa visima, hususan visima vifupi.

(iii). Upungufu wa mvua unaweza kuathiri upatikanaji wa malisho na maji kwa ajili ya mifugo

#### Ushauri

(i). Wakulima wanashauriwa kuandaa mashamba, kupanda, kupalilia na kutumia pembejeo husika kwa wakati na kuchagua mbegu na mazao sahihi.

(ii). Wakulima wanashauriwa kutumia mbinu bora za kilimo zinazohifadhi unyevunyevu katika udongo.

(iii). Wafugaji wanashauriwa kutumia mbinu bora za ufugaji ili kutunza malisho na kuvuna maji ya mvua kwa matumizi ya baadae.

(iv). Wafugaji wa samaki wanashauriwa kuimarisha miundombinu ya ufugaji.

Utabiri wa hali ya hewa nchini na tahadhari zinapatikana katika tovuti ya Mamlaka: **www.meteo.go.tz**

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz